

Wilson



Utambulisho:

Naitika kwa jina ya Wilson.

Anwani:

Minaishi katika kambi ya wakimbizi ya Bulengo kunaisha miezi tatu. Nikikimbia vita ya vikundi vya waasi wa silaha Masisi.

Kuanza kwa vita:

Nakumbuka iyo vita kati ya makundi yenye silaha ilipoanza, nilikuwa na miaka munane, ikaendelea mpaka/hadi leo na ndiyo iliacha minakimbia.

Matokeo ya vita:

Vita ilipokuya, ilikuwa ikitafuta watu wamoya wamoya, ao eneo fulani fulani. Wanapofika wanakuwa wa eneo fulani, wanaenda tafuta watu kutoka eneo fulani (lingine lolote). Kwa hiyo, unapo mwona mtu wa eneo/mtaa fulani au eneo fulani, unakumbuka, unaona kama hakuna kitu kingine kinamuleta, ni wewe anakuya kutafuta ili akuue.

Iyo vita iliniletewa na matokeo kazaa kwenye maisha yangu ya kibinafsi, sikusoma vizuri, tulikimbia, masomo/shule ikafungwa, na kwa jamaa, nikapoteza mzazi niliyempenda, piya na marafiki zangu. Kwa ujumla, vitu vilibiwa, nyumba zikalungula/zilichomwa, hatuendi tena mashambani, kulikuwa na njaa mingi katika jamii, na pia tukaogopa kurudi nyumbani; tukakuwa katika ukimbizi na kulala ndani ya pori. Kuhusu elimu ya watoto, masomo ilifungwa, yengine ya shule yalibomolewa na kukongwa/kuchomwa moto, na watoto waliishi mitaani, wakakosa namna ginsi yakusoma, hata kwa hiyo wamoya wamoya wakaingiya/walijiunga na vikundi vyenye silaha.

Tatizo niliopata kimafikiri/kiakili, ni pale nilipopanga kusoma, miaka ilisogeya nyuma na ikawa ndefu. Wakati Ninapomwona mmoja wa wale waliokuwa sehemu ya vikundi hivi vilivyo na silaha, ninakumbuka mambo niliyopitia mbele/hapo awali. Hiyo vita kwa kiakili, iliachanakuwa na woga ninapokumbuka niliyopitia, watu waliouawa, nyumba zilizolunguzwa/zilizochochomwa moto, na watu waliolunguzwa/waliochochomwa moto ndani ya manyumba. Na wakati tunaposikia kelele fasi fulani, unawaziya/unafikiria yakuwa/kwamba hao makundi haya yenye silaha wanarudiya inakumbusha mambo uliyo pitiya. Ninapo sinziya, huwa sisinziye vizuri, kwani ninapolala naota matukio yaliyopita. Kwa mfano, wakati ninapo ona gari linapita, inafaa ajali ninakumbusha watu niliowaona walio katakatwa hai kwa hiyo vita. Kwa hiyo sasa ninahisi kama siko huru. Katika maisha yangu, ninapona vitendo hivi, nakumbuka mambo mengi sana, na maendeleo yangu hupungua polepole. Ninaposoma, kuna wakati nakumbuka bitu iliyonipitiya/matukio niliyopata, na wakati nikisoma kitabi nafika katikati, napatwa na woga na kuacha kusoma. Au ninapopanga mradi fulani, ninapofika katikati, nikikumbuka mambo iliyoharibika siku zilizo pita, naacha kuendelea na mradi huo.